**2018** **MULIKA NA. 37**


**TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI**
**CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM**



**MHARIRI MKUU**
**M.M. MULOKOZI**

**MHARIRI MSAIDIZI**
**MUSSA HANS**

© TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI

**KAMATI YA UHARIRI**

| | | |
|---|---|---|
| Dkt. Ernesta Simon Mosha | - | Mkurungenzi, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| Prof. Mugyabuso M. Mulokozi | - | Mhariri Mkuu |
| Dkt. Mussa Hans | - | Mhariri Msaidizi |
| Dkt. Lutz Diegner | - | Chuo Kikuu cha Humboldt (Ujerumani) |
| Dkt. Athumani Ponera | - | Chuo Kikuu cha Dodoma (Tanzania) |
| Dkt. Miriam Kenyani Osore | - | Chuo Kikuu cha Kenyatta (Kenya) |

**WASHAURI WA WAHARIRI**

| | | |
|---|---|---|
| Prof. Cyprean Niyomugabo | - | Chuo Kikuu cha Rwanda (Rwanda) |
| Prof. Sangai Mohochi | - | Chuo Kikuu cha Rongo (Kenya) |
| Dkt. Abel Mreta | - | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Tanzania) |
| Dkt. Joseph Nyehita Maitaria | - | Chuo Kikuu cha Karatina (Kenya) |
| Dkt. S.S. Sewangi | - | Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) |
| Prof. Ipara Odeo | - | Chuo Kikuu cha Kibabii (Kenya) |
| Dkt. Wael Nabil Ibrahim | - | Chuo Kikuu cha Al Azhar (Misri) |

**ADA KWA MWAKA**

| | | |
|---|---|---|
| Afrika Mashariki | - | Shilingi za Kitanzania 5,000 |
| Kwingineko | - | Dola za Kimarekani 40 (kwa ndege) |

**Habari za Mkondoni**

Jarida hili linapatikana pia mkondoni kupita tovuti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam www.udsm.ac.tz. Aidha, utaratibu wa kuingiza jarida hili katika tovuti ya majarida ya Afrika mkondoni AJOL uko ukingoni. Utaratibu huu utakapokamilika jarida hili litapatikana katika www.ajol.info.

**Kwa mawasiliano tumia anwani ifuatayo:**
**Mhariri Mkuu,**
**MULIKA,**
**S.L.P. 35110,**
**Dar es Salaam,**
**Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**.

Maoni yaliyomo kwenye jarida ni ya wenye makala na si lazima yakubaliane na yale ya Wahariri au Kamati ya Uhariri ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

## MAELEKEZO KWA WAANDISHI NA UTARATIBU WA KUTATHMINI MAKALA

MULIKA ni jarida la taaluma ya Lugha na Fasihi ya Kiswahili. Jukumu lake kuu ni kukusanya na kusambaza maarifa yanayohusu Lugha na Fasihi ya Kiswahili yaliyokitwa katika utafiti mpevu. MULIKA limeendelea kuwa daraja kati ya watumiaji wa Kiswahili popote walipo, na wataalamu wa Kiswahili katika shule za Sekondari na Vyuo vya Elimu ya Juu Afrika ya Mashariki.

Jarida huchapishwa mara moja kwa mwaka.

Jarida linapokea makala yaliyoandikwa kwa Kiswahili TU. Makala yapigwe chapa kwenye karatasi za A4, mistari ikitengwa kwa kipimo cha nafasi mbili. Upande mmoja tu wa karatasi utumiwe.

Mwandishi awasilishe kwa Mhariri, nakala tatu za muswada wake, pamoja na nakala tepe iliyowekwa katika mfumo wa Kikompyuta katika muundo wa Microsoft WORD.

Ukurasa wa kwanza wa makala uoneshe jina la makala, jina kamili la mwandishi (au waandishi) wa makala (ikiwa ni pamoja na wadhifa wake) na anwani yake.

Ukurasa wa pili uoneshe jina la makala na ufupisho wa makala (Ikisiri) kwa maneno yasiyozidi 300. Jina la mwandishi lisiandikwe.

Unapotaja marejeleo kwenye matini, taja jina la mwisho la mwandishi, likifuatiwa katika mabano na tarehe ya chapisho lake na kurasa zilizorejelewa, k.m. Yahya (1983:139). Kwenye orodha ya marejeleo au bibliografia majina ya warejelewa yapangwe kialfabeti.

Tanbihi ziwekwe namba na zitumike pale tu inapobidi. Maelezo ya tanbihi yatolewe kwenye ukurasa wa pekee mwisho wa makala, yaani kabla ya kuorodhesha marejeleo.

Makala yatatathminiwa na walau wasomaji wawili ambao hawatapewa taarifa za mwandishi. Mwandishi atajulishwa matokeo ya tathmini ya makala yake ndani ya miezi mitatu (3) tangu kupokewa kwa makala hayo. Makala yaliyokataliwa hayatarejeshwa kwa waandishi. Waandishi ambao makala yao yatakubaliwa kuchapishwa watajulishwa kwa maandishi kuwa makala yao yamekubaliwa kuchapishwa katika Juzuu husika.

# YALIYOMO

Tahariri........................................................................................................ v

**Euphrase Kezilahabi kama Mwanafalsafa Kamili: Mifano Kutoka Riwaya ya *Mzingile***
Wallace Mlaga................................................................................... 1

**Ufutuhi katika Jamii za Watanzania: Mjadala kuhusu Sura za Utokeaji na Dhima zake**
A.S. Ponera......................................................................................... 23

**Dhana ya Zubu katika Nyimbo za Harusi za Waswahili: Uchambuzi wa Kisaikolojia Changanuzi**
Issa Mwamzandi.................................................................................. 45

**Fasihi Tafsiriwa za Kigeni: Urafiki au Uadui kwa Fasihi ya Kiswahili**
Joseph Nyehita Maitaria; Peter M. Kinyanjui na Leah Mwangi........ 59

**U-Nigeria: Athari zake katika Filamu za Kiswahili nchini Tanzania**
G.A. Kasiga.................................................................................... 72

**Athari za Mgawanyo Tofauti wa Majukumu ya Kijinsia katika Nyimbo za Watoto kwa Watoto**
Doroth F. Mosha.............................................................................. 87

**Tungo za Mrisho Mpoto: Sitiari ya Mwenendo wa Siasa na Utawala Nchini**
Manyuka Majuto Kapaya.................................................................. 106

**Mpaka kati ya Uganga na Uchawi: Uchunguzi kutoka Riwaya za Kiethnografia za Kiswahili**
Lameck Mpalanzi.............................................................................. 130

**Ukiukwaji wa Nadharia Tumizi ya Uakifishaji katika Kazi za Kitaaluma za Wanafunzi wa Shule za Msingi Tanzania**
Rehema Stephano.............................................................................. 151

**Mtindo katika Hotuba za Rais J.P. Magufuli na Mchango wake katika Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili**
Ahmad Y. Sovu…………………………………………………..... 169

# TAHARIRI

Kwa mara nyingine Jarida la *Mulika* ambalo ni miongoni mwa majarida yanayotolewa na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam linakuletea makala mbalimbali ya kitaaluma. Toleo hili Na. 37 la mwaka 2018 limesheheni makala mbalimbali yahusuyo fasihi, isimu na lugha ya Kiswahili. Wakati taaluma za Kiswahili zikizidi kupata mashiko na kusambaa kote duniani katika ngazi mbalimbali za kitaaluma, umuhimu wa maandiko ya taaluma hizo unazidi kuongezeka pia. Kwa hivyo, pasi na shaka jarida hili adhimu, kupitia makala zilizomo litatoa mchango mkubwa kwa walimu, wanafunzi na wapenzi wengine wa Kiswahili.

Toleo hili la *Mulika* limebeba makala ambayo kwayo kila mwandishi amejitahidi kuogelea kwa mapana na marefu katika kutoa taaluma ya eneo maalumu alilolishughulikia. Wallace Mlaga anaandika kuhusu "Euphrase Kezilahabi kama Mwanafalsafa Kamili: Mifano kutoka Riwaya ya *Mzingile."* Anaeleza kuwa badala ya kumwona Kezilahabi kama mwandishi anayeshughulikia masuala ya kifalsafa kupitia kazi zake, kwa namna anavyoyashughulikia masuala hayo na kutaka jamii iwe na mtazamo mpya, anapaswa kuitwa mwanafalsafa kamili. Makala ya "Ufutuhi katika Jamii za Watanzania: Mjadala kuhusu Sura za Utokeaji na Dhima zake," yameandikwa na A.S. Ponera. Mwandishi anaonesha namna ufutuhi unavyojitokeza katika jamii na dhima yake. Anafanya hivyo kwa kutumia data mbalimbali za ujumbe wa maandishi. Naye Issa Mwamzandi ameandika kuhusu "Dhana ya Zubu katika Nyimbo za Harusi za Waswahili: Uchambuzi wa Kisaikolojia Changanuzi." Makala haya ya aina yake yahusuyo ufeministi yamechambuliwa kwa mtazamo wa saikolojia changanuzi.

Joseph Nyehita Maitaria, Peter M. Kinyanjui na Leah Mwangi wanakuletea makala ya "Fasihi Tafsiriwa za Kigeni: Urafiki au Uadui kwa Fasihi ya Kiswahili." Katika makala haya waandishi wanaonesha historia ya kazi za kifasihi zilizofasiriwa kutoka lugha za kigeni kwenda katika Kiswahili. Wanahoji ikiwa fasiri za aina hiyo ziendelee kuwapo baada ya fasihi ya Kiswahili kukua. Pia, wanaonesha faida na hasara za kazi hizo. Makala ya "U-Nigeria: Athari zake katika Filamu za Kiswahili nchini Tanzania" yanaletwa kwako na G.A. Kasiga. Mwandishi katika makala haya anaonesha athari za U-Nigeria katika filamu za Kiswahili nchini Tanzania. Anaenda mbali zaidi kuonesha athari za suala hilo katika utamaduni wa Watanzania kwa sura chanya na hasi. Makala ya "Athari za Mgawanyo Tofauti wa Majukumu ya Kijinsia katika Nyimbo za Watoto kwa Watoto" yameandikwa na Doroth Mosha. Makala haya yanaangazia madhara ya nyimbo za watoto – namna zinavyoweza kuathiri mitazamo yao katika mustakabali wa majukumu na maendeleo yao. Manyuka M. Kapaya anaandika kuhusu "Tungo za Mrisho Mpoto: Sitiari ya

Mwenendo wa Siasa na Utawala Nchini." Mwandishi anaziangalia tungo za msanii huyu kama zilizosheheni sitiari aitayo ya mwenendo wa kisiasa. Naye Lameck Mpalanzi anaandika kuhusu "Mpaka kati ya Uganga na Uchawi: Uchunguzi kutoka Riwaya za Kiethnografia za Kiswahili." Mwandishi kwa kupitia jicho la kifasihi anajaribu kuonesha mpaka kati ya uganga na uchawi.

Rehema Stephano na Ahmad Sovu wanaandika katika uga wa isimu na matumizi ya lugha. Stephano anatanabahisha kuhusu "Ukiukwaji wa Nadharia Tumizi ya Uakifishaji katika Kazi za Kitaaluma za Wanafunzi wa Shule za Msingi Tanzania." Mwandishi kwa kutumia nadharia shadidi anaonesha namna makosa mbalimbali yanavyojitokeza katika uandishi kutokana na kukiukwa kwa uakifishaji. Anaonesha namna ambavyo alama za uakifishi zinapaswa kuzingatiwa. Sovu anaandika kuhusu "Mtindo katika Hotuba za Rais J.P. Magufuli na Mchango wake katika Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili." Katika makala haya mwandishi anaonesha mitindo mbalimbali katika hotuba za Rais Magufuli na dhima ya mitindo hiyo. Kadhalika, anaonesha mchango wa Rais katika ulimwengu wa Kiswahili kutokana na anavyokienzi katika matumizi ya kila siku.

Tunatumaini kwamba wasomaji wetu popote walipo watanufaika na makala ya toleo hili la *Mulika*. Hata hivyo, makala haya si misahafu. Changamoto zitakazopatikana katika usomaji zisaidie kuzua mjadala utakaozaa makala mengine ya kitaaluma katika jarida hili. Tunakutakia usomaji mwema.

**Wahariri**